

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA FEDHA  
NA MIPANGO

Wakala wa Huduma ya Ununuzi  
Serikalini (GPSA)



**MFUMO WA UNUNUZI WA VIFAA  
NA HUDUMA MTAMBUKA**

---

## **1.0 UTANGULIZI**

Mfumo wa ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka (VHM) ni mfumo rafiki unaowajumuisha wafanyabiashara na wazalishaji mbali mbali ndani ya nchi kwa kuwaratibu kwa mujibu wa sheria na miongozo ya ununuzi wa Umma kwa lengo la kuwawezesha kuuza vifaa na huduma zao kwenye Taasisi za Umma kuititia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA).

Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) unatekeleza mfumo wa ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka kwa mujibu wa kifungu Na. 50 kanuni ya 131 ya sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016. Wakala (GPSA) unaelekezwa kwa mujibu wa kifungu tajwa kuandaa mfumo wa ununuzi wa pamoja wa vifaa na huduma mtambuka kwa kutumia mikataba maalumu kwa ajili ya taasisi nunuzi.

Lengo la mfumo wa ununuzi wa pamoja wa vifaa na huduma mtambuka ni kupunguza gharama (fedha na muda) na kuongeza ufanisi katika uhitaji wa vifaa na huduma mtambuka (zinazohitajika mara kwa mara) kwenye taasisi za umma kwa kuwatumia wazabuni wenye mikataba maalum.

---

---

## **2.0 WADAU WAKUU KATIKA MFUMO HUU WA UNUNUZI**

- 2.1 Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma [PPRA]
- 2.2 Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini [GPSA]
- 2.3 Taasisi za Ununuzi
- 2.4 Wazabuni wa Vifaa na Huduma Mtambuka

## **3.0 FAIDA ZA MFUMO**

### 3.1 Faida kwa taasisi za ununuzi

- i. Kuondoa tofauti kubwa ya bei ya vifaa na huduma baina ya taasisi moja na nyingine.
- ii. Kutoa nafasi kwa taasisi nunuzi kujihusisha zaidi na majukumu ya msingi ya taasisi husika, kwa mfano wizara ya Elimu kushughulikia masuala ya kuongeza tija katika utoaji elimu bora.
- iii. Kupunguza muda wa kupata vifaa .
- iv. Kuwezesha taasisi za serikali kutekeleza mipango yao kwa kuzingatia matumizi sahihi ya fedha za umma kwa mujibu wa sheria na kanuni za ununuzi sanjari na sheria za fedha za umma.
- v. Kuondoa mianya ya rushwa kwa kuimariswa uwazi wa taasisi nunuzi kuwatumia wazabuni walioandaliwa baada ya kukidhi vigezo.

---

### 3.2 Faida kwa wazabuni ni pamoja na :-

- i. Kutoa fursa sawa kwa wafanyabiashara wa ngazi zote katika ushiriki wa zabuni.
- ii. Mikataba maalumu hutolewa kwa kufuata maeneo na hivyo kutoa uhuru kwa wazabuni kuomba maeneo watakayo.
- iii. Kuokoa muda na fedha katika ushiriki wa mchakato wa zabuni.
- iv. Habari za kina kuhusu zabuni hupatikana kwa urahisi katika kituo kimoja [GPSA]
- v. Kuongeza uwazi na usawa kwenye mchakato wa zabuni na kupelekea kuondoa rushwa na urasimu.
- vi. Kupata elimu namna ya ushiriki wa zabuni zenye kushindanishwa Kitaifa (National Competitive Tendering)
- vii. Fursa ya soko kwa wazalishaji wa ndani ya nchi ili kutekeleza kwa vitendo azma ya sera ya viwanda.

---

#### **4.0 ORODHA YA VIFAA NA HUDUMA MTAMBUKA**

Orodha ya Vifaa [Items] Mtambuka ni kama ifuatavyo:-

No.	CLASS	DESCRIPTION
1.	A	Stationery and Office Supplies
2.	B	Office Equipment and Consumables
3.	C	Furniture and Fittings
4.	D	Cleaning Materials and Supplies
5.	E	Non consultancy services
6.	F	Motor Vehicle Accessories
7.	G	Food and Beverages
8.	H	Uniforms, Beddings, Sports Gears and Textile Materials
-----		
9.	I	Laboratory Supplies
10.	J	Kitchen Appliances
11.	K	Building Materials, Machinery and Hardware
12.	L	Firewood and Charcoal
13.	M	Fuel and Lubricants

---

Orodha ya Huduma Mtambuka [NON CONSULTANCY SERVICES]  
ni kama ifuatavyo:-

NA.	CLASS	DESCRIPTION
1.	E - 01	Catering Services
2.	E - 02	Cleaning Services
3.	E - 03	Fumigation Services
4.	E - 04	Transport and Handling Services
5.	E - 05	Service and Maintenance of Office Equipment
6.	E - 06	Service and Maintenance of Firefighting Equipment
7.	E - 07	Grinding and Milling
8.	E - 08	Provision of Maintenance and Service of Elevator
9.	E - 09	Service and Maintenance of Fire Security Systems
10.	E - 10	Hiring Photocopying Services using Vendor Management Inventory System
11.	E - 11	Internet Services
12.	E - 12	Documentary Services
13.	E - 13	Insurance Brokerage Services
14.	E - 14	Security Services

---

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:-

Mtendaji Mkuu

Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA)

Mtaa wa Bohari na Barabara ya Nyerere,

Eneo la Keko Mwanga,

S.L.P 9150,

Dar es Salaam

Simu: +255 22 286 6071/286 1617

Nukushi: +255 22 286 6072

Tovuti: [www.gpsa.go.tz](http://www.gpsa.go.tz)

Barua pepe: [ceo@gpsa.go.tz](mailto:ceo@gpsa.go.tz)

